

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Pili – Tarehe 2 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mheshimiwa Ghati Chomete, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 1

Agizo la Rais la Kukarabati Stendi Bweri - Musoma

MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MHE. GHATI Z. CHOMETE Aliuliza:-

Je, ni lini agizo la Mheshimiwa Rais la kuboresha stendi ya Bweri Musoma Mjini litatekelezwa?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) Alijibu:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali kwa ridhaa yako naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Baraka kwa kutujaalia afya njema sisi sote na kutuwezesha kuendelea na majukumu haya ya kuwatumikia watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa aliyonipa na kuteua kuendelea kuwatumikia watanzania wenzetu katika dhamanahii muhimu ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Naomba kumuahidi Mheshimiwa Rais kwamba nitafanya kazi kwa bidii yangu yote ili kuhakikisha imani yake na maono wake ya kuwatimizia maendeleo watanzania yanatimia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya utangulizi, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, stendi ya mabasi ya Bweri katika Manispaa ya Musoma ilijengwa mwaka 2007 kwa mapato ya ndani ya halmashari kwa kutumia Mkandarasi CMG *Construction Company Ltd* aliyeingia mkataba wa shilingi bilioni 1.36 ambapo Mkandarasi huyo alifanya kazi zenye thamani ya shilingi milioni 921.17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa stendi hiyo yenye uwezo wa kuingiza magari 35 hadi 45 ina miundombini iliyochakaa hivyo inahitaji kuboreshwa. Kwa kutambua umuhimu wa stendi hiyo, tayari Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imeandaa andiko la mradi huo na limewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya Uchambuzi wa kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi kupitia ufadhili wa Benki ya *BADEA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utaratibu wa kupata ufadhili huo ili mradi huo pamoja na miradi mingine inayotarajiwa kutekelezwa kupitia ufadhili huo utekelezaji wake uweze kuanza. Ahsante.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tunza I. Malapo swalii la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa mujibu wa muuliza swalii alitaka kujua ni lini Mheshimiwa Waziri hajajibu. Sasa na naendelea kuuliza ni lindi stendi hiyo itaboreshwaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii langu la pili, tatito lililopo katika stendi hiyo ya Bweri Musoma ni sawa kabisa na tatizo ambalo lipo katika stendi ya Mkoa katika Jimbo la Mtwara Mjini, stendi ipo eneo linaitwa Mkanaleli. Stendi ile ni mbaya sasa hivi mvua zinaponyesha maji yanatuama.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inaboresha stendi ile iendane na viwango kama zillivyo stendi katika mikoa mingine na majimbo mengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi nimesema kwamba Serikali tayari imeanza mazungumzo na Benki ya *BADEA* ili kupata ufadhili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi ya Bweri katika Manispaa ya Musoma Mjini, na ujenzi huo utaanza wakati wowote mara fedha hizo zitakapopatikana.

Kwa hiyo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wakati wowote fedha hizo zikipatikana kazi ya ujenzi wa stendi ile utaanza mara moja.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kuhusiana na stendi ya Mkanaleli naomba nimpe wito Mheshimiwa Mbunge lakini pia niwaelekeze Mamlaka za Serikali za Mitaa kwamba, miundombinu hii yote stendi lakini na miundombinu mingine ipo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, wanawajibika kuhakikisha wanatenga bajeti kujenga au kukarabati stendi hizo lakini kama uwezo wa kibajeti hautoshelezi kutenga bajeti hizo basi wanaelekezwa kuandaa maandiko maalum kwa maana ya maandiko ya kimkakati ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe wito kwa halmashauri hiyo kuhakikisha wanafanya tathmini mara moja ya uhitaji wa ujenzi wa stendi hiyo na kuona uwezo wao wa kujenga lakini kuomba miradi ya kimkakati ili Serikali iweze kusaldia kujenga stendi hizo. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Seif K. S. Gulamali Mbunge wa Manongo.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kwa niaba ya wananchi wa Manonga wanapenda kupongeza kuchaguliwa kwa Mheshimiwa Dkt.Tulia Ackson kuwa Mwenyekiti, wa Bunge letu. Lakini kwa niaba pia ya Wananchi wa Manonga naomba sasa swali langu Na. 2 liweze kupatiwa majibu. Ahasante.

Na. 2

Utekelezaji wa Ahadi ya Rais-Manonga

MHE. SEIF K. S. GULAMALI Aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Kata ya Ziba Wilayani Igunga aliyoitao wakati wa Kampeni za uchaguzi 2020.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISMEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif K. S. Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kujenga Vituo vya kutolea Huduma za Afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha utolewaji wa Huduma ya Afya ya Msingi kwa Wananchi. Ujenzi na Ukarabati wa Vituo unahusisha utekelezaji wa ahadi za viongozi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kutekeleza mkakati huu Serikali imepeleka kiasi cha shilingi bilioni 58.25 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vipyta vya afya 233 katika Tarafa na Kata za kimkakati ambazo hazikuwa na miundombinu hiyo. Aidha, Serikali imepeleka shilingi milioni 250 katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Ziba ambapo ujenzi umefikia hatua ya umalizaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkakati huu Serikali itaendelea kutoa fedha katika Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi za viongozi za kujenga au kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Seif Gulamali swali la nyongeza.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali ya Chama cha

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mapinduzi kwa kuweza kutekeleza ahadi za Viongozi wa Kitaifa hasa ilikuwa ni ahadi ya kipindi cha kampeni 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu nipende tu kuuliza kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa amekuja pale Chomachankola. Nilikuwa naomba pia kuweza kupata jibu juu ya Kituo cha Afya cha Chomachamkola ambacho Mheshimiwa Waziri Mkuu alituahidi kutupatia fedha kwa ajili ya kujenga majengo ya wazazi pale. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Seif Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Seif Gulamali kwa kuwasemea kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo la Manonga na ufuatiliaji wake kuhakikisha Serikali inaendelea kuwalettea maendeleo wananchi wa jimbo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nipokee shukrani zake nyingi kwa Serikali na kwa kweli sisi sote Waheshimiwa Wabunge tumeona kazi kubwa sana inayofanywa na Serikali katika kuboresha miundombinu ya huduma za afya na ndani ya hii miezi sita Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amepeleka zaidi ya bilioni 58 na milioni 250 kujenga Vituo vya Afya 233 kote Nchini. Kwa hivyo, tunapokea shukrani hizi na tuwahakikishie kwamba tutaendelea kushirikiana naye kuhakikisha tunaendelea kuboresha miundombinu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la Kituo cha Afya ambacho ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimuhakikishie kwamba ahadi zote za Viongozi wetu wa Kitaifa zinapewa kipaumbele ikiwemo kituo hiki cha Afya tutaendelea kutafuta fedha na mara zikipatikana

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tutakwenda kuhakikisha kwamba tunaanza ujenzi wa Kituo cha Afya hicho. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Musukuma nimekuona.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, matatizo yaliyopo katika Jimbo la Manonga ni sawa kabisa na matatizo yaliyopo kwenye Jimbo la Geita. Kata ya Nkome ina zahanati ambayo kwa mwezi inazalisha watoto wasiopungua 400 na Mheshimiwa Naibu Waziri amefika pale Silinde. Mheshimiwa Waziri juzi tu tumefika ukajiona hali halisi chumba kidogo ukakuta kinamama zaidi ya wanenye wanjifungua pale. Sasa nimeshauliza humu mara mbili mara tatu ninapata tu ahadi ambazo hazijatekelezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kupata majibu ya uhakika kwamba ni lini sasa kwa kuwa Mawaziri wote wamefika pale mtanipa fedha ya dharula ili niweze kuwaokoa wale wananchi wa Kata ya Nkome? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Musukuma, kwanza naomba unipe nafasi nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu, kwa kunipa majukumu ya kumsaidia katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Rais wetu kwamba, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitatumia maarifa na jitihada zote na kwa ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge naamini mtanipa ushirikiano ili nisiveze kumwangusha Mheshimiwa Rais wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Musukuma kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli siku si nyingi niliambatana na Mheshimiwa Musukuma kwenda kwenye Jimbo lake la Geita Vijijini. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Musukuma kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwatetea wananchi wake wa Geita Vijijini. Kama nilivyomuahidi Mheshimiwa Musukuma tukiwa Geita Vijijini, muda wowote Serikali tukipata fedha tutaangalia namna ya kuboresha Zahanati ya Nkome ili iweze kuwa Kituo cha Afya ili wananchi wa Kata Nkome pamoja na maeneo ya jirani waweeze kupata huduma nzuri kwa mujibu wa Sera ya Kituo cha Afya. Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Jesca J. Msambatavangu aulize swali lake.

Na. 3

Serikali Kurejesha *Moving Expenses* kwa Watumishi wa Umma

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU Aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha kipengele cha “*moving expenses*” kilichotolewa ili watumishi walipwe fedha za nauli wakati wakisubiri mafao mengine?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni J(1) na J(8) ya Kanuni za Kudumu Katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

pamoja na Waraka wa Utumishi Na. 5 wa mwaka 2008, kipengele cha *moving expenses* hakijaondolewa. Hivyo, Serikali imekuwa ikigharamia usafiri yaani nauli kwa watumishi wa umma kwa kuzingatia utaratibu ulioelezwa kwa kuzingatia Kanuni tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni J(6)(1) ya Kanuni za Kudumu Katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 Mtumishi wa Umma hulipwa gharama za usafiri yaani nauli, yeye, mwenza wake na watoto au wategemezi wasiozidi wanne wenye umri chini ya miaka 18 pale anapoajiriwa, anapohama au utumishi wake unapokoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haki ya kila mtumishi anapostaafu kulipwa gharama za usafiri kurudi mahala atakapoishi baada ya kustaafu, ni wajibu wa kila mwajiri kuhakikisha anatenga fedha za "*moving expenses*" kwenye bajeti. Hivyo, nitumie nafasi hii kuwakumbusha na kuwataka waajiri kutenga fedha hizi na kutekeleza wajibu wao. Aidha, nichukue fursa hii kuwataka waajiri wote kuandaa orodha ya watumishi wanaokaribia kustaafu na hivyo kurahisisha kubaini gharama halisi zitakazohitajika kuwasafirisha na kuzitenga kweye bajeti kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kanuni J(8) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 pamoja na Waraka wa Utumishi Na. 5 wa mwaka 2008 kuhusu usafirishaji wa mizigo yaani *personal effects* ya watumishi wa umma, imeeleza namna ya kusafirisha mizigo ya mtumishi wa umma pale anapohama au utumishi wake unapokoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kulipa gharama za kusafirisha watumishi wa umma, familia zao pamoja na mizigo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca swal la nyongeza.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nilikuwa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza je, Serikali iko tayari sasa kuweka utaratibu wa muda maalum kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hizo *moving expenses* zinalipwa ili kuondoa usumbufu kwa watumishi wa umma?

Lakini swalii langu la pili je, ni lini sasa Serikali pia itafanya marekebisho kwa yale madaraja ya watumishi wa umma yaliyofutwa mwaka 2016 na 2017. Hasa katika Manispaa yangu ya Iringa wapo watumishi zaidi ya 300 ambaao hawajafanyiwa marekebisho pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyiwa na Serikali ya kupandisha madaraja. Ni lini itafanya kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pia tumeshaleta sana hili ombi mara nyingi sana kwa Waziri lakini halijafanyiwa kazi, tunaomba *commitment* ya Serikali? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kwanza kama nilivyo sema kwenye majibu ya msingi. Waajiri wote wanatakiwa kuhakikisha wanatekeleza matakwa ya Kanuni za Kudumu za Kudumu za Utumishi wa Umma na tayari Kanuni hizo zipo kwamba ni Mtumishi yoyote anapokoma utumishi wake wa umma au mtumishi pale anapohama anastahili kulipwa *moving expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitumie fursa hii kuwataka tena Waajiri kuhakikisha wanatenga bajeti ya *moving expenses* kwa sababu wanajulikana wale watumishi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ambao wanakaribia kustaafu. Sasa ni wajibu wa mwajiri kuangalia wale wanaokaribia kustaafu mwaka unaofuata wa fedha na kuweza kutenga bajeti hiyo. Kwa hiyo, nirudie tena kuwataka Waajiri wote si tu wa *local government*, si tu wa Iringa Mjini, lakini taasisi zote za umma kuhakikisha wanatenga bajeti kwa ajili ya watumishi wao katika hii *moving expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye swali lake la pili, la madaraja ya 2006. Madaraja haya yalisimama kuanzia Mei, 2016 lakini madaraja haya yalianza tena kutolewa mwezi Novemba, 2017 ambapo Serikali ilipandisha jumla ya watumishi 55,000 Novemba, 2017. Hii ya kutoka 2016 madaraja haya yalikoma kupisha uhakiki uliokuwa ukiendelea, lakini sasa tunaangalia ni namna gani bora ya kuweza kuleta msawazo ili kulindi ile *Seniority* katika eneo la kazi na Serikali bado inalfanya kazi suala hilli na litakapokuwa tayari tutatolea maelezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante sana tunaendela na Wizara ya Maji, sasa Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Mwibara aulize swali lake.

Na. 4

Huduma ya Maji Safi na Salama – Mwibara

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza dhamira yake ya kuwatua Wanawake ndoo kichwani kwa kuwasogezee huduma za maji safi na salama karibu na makazi yao katika Jimbo la Mwibara?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuamini sisi Wizara ya Maji. Nataka niahidi Waheshimiwa Wabunge na watanzania mimi Jumaa Aweso na timu nzima ya Wizara ya Maji, hatutokuwa kikwazo kwa watanzania kupata maji safi, salama na yenze kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya timu nzima ya Menejimenti ya Wizara ya Maji tunatoa pongozi kwa Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson kwa kuaminiwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi Wizara ya Maji tutatoa ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha tunafanikisha Bunge hili letu tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajenge, Mbunge wa Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Serikali ni kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi ni ya uhakika na endelevu. Kwa sasa, upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Bunda ambapo Jimbo la Mwibara lipo wastani wa asilimia 69 kuititia visima virefu na vifupi 237 vya pampu za mkono, chemchemi moja na skimu za mtandao wa bomba tano.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tupunguze sauti tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali inaendelea na mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Mwibara kwa kutekeleza miradi mipya ya Buzimbwe, Bulendabufwe, Igundu, upanuzi wa mradi wa maji Iramba kwenda vijiji vya Mugara, Nyarugoma na Muhura. Kazi zinazofanyika kwa miradi mipya ni pamoja na ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa litu 135,000, ujenzi wa vituo 28 vya kuchotea maji, ujenzi wa ofisi moja ya jumuiya ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

watumiaji maji na ujenzi wa nyumba ya mitambo (*pump house*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kazi zinazofanyika kwa mradi wa upanuzi ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa Kilometra 18.6, ununuzi na ufungaji wa pampu mpya (*surface pump*). Miradi hii kwa sasa imefikia wastani wa asilimia 15 za utekelezaji na inatarajia kukamilika mwezi Juni, 2022. Kukamilika kwa miradi hii kutaboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Bunda inapatiwa ufumbuzi wa kudumu, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 itakamilisha usanifu wa mradi wa maji wa Kisorya kupitia chanzo cha maji cha Ziwa Vicktoria. Mradi huo umepangwa kuhudumila vijiji 12 vya Sunsi, Masahunga, Kisorya, Nambubi, Mwitende, Nansimo, Nambaza, Busambara, Mwibara, Kibara A, Kibara B na Kasahanga. Ujenzi wa mradi unatarajia kutekelezwa kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 baada ya usanifu kukamilika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Charles Kajege swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kumtua mama ndoo kichwani mradi mkubwa ambao utasababisha hili litokee ni mradi wa Miji 26 ambao unafadhiliwa na Serikali ya India. Tunaomba kuuliza Mheshimiwa Waziri.

Ni lini mradi huu utaanza na umefikia wapi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge lakini kama unavyotambua *program* ya kumtua mwana mama ndoo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kichwani ni programu ya Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maji kupitia bajeti ya Serikali lakini kupitia wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Serikali ya India tunatarajia kutekeleza miradi ya Miji 28 zaidi ya dola milioni 500 na mpaka sasa hatua ambayo tumefikia taratibu zote za kimanunuzi kama Wizara ya Maji tumeshazikamilisha. Tunasubiri kibali (*no objection*) kutoka *Exim Bank* na hivi karibuni tutapata, katika kuhakikisha tunatekeleza miradi hiyo na wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama.

MWENYEKITI: Nimemuona Mheshimiwa Samwel Hhayuma na halafu Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. SAMWEL X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Changamoto ya maji inayoikumba Jimbo la Mwibara ni sawasawa na ambayo tunaipata kwenye Mkoa wetu wa Manyara na sehemu kubwa huwa tunapata changamoto kubwa hasa kwenye eneo la kuchelewa kwenye suala la manunuzi. Pale Mkoani hatuna Afisa Manunuzi.

Je, Wizara iko tayari kwa kushirikiana na Utumishi kupeleka Afisa Manunuzi pale Mkoani ili kuharakisha manunuzi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Hanang kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Jimbo lake. Sisi kama Wizara ya Maji tutaendelea kumpa ushirikiano katika kuhakikisha tunatatua matatizo ya maji katika Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la Maafisa Manunuzi ni kweli tumeanzisha Taasisi yetu ya (RUWASA) Wakala wa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Maji Vijijini, hii ni mahususi kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji vijijini. Lakini tumekuwa na changamoto ya watumishi hususani katika eneo la manunuzi. Tumeshafanya mazungumzo na wenzetu wa Utumishi na hivi karibuni tutapata Maafisa hao katika kuhakikisha tunakwenda kutatua matatizo ya maji. Eneo ambalo tutalipa kipaumbele kabisa ni Mkoa wa Manyara katika kuhakikisha hii changamoto tunaifanikisha kwa haraka. Ahsante sana. (Makof)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya na pia nimemuona Mheshimiwa Assa Makanika.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa moyo wa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Aweso, kwetu sisi amejitahidi kuutendea haki Mradi wa Bunda umepiga hatua. Sasa ningependa kuuliza swali la nyongeza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji yametoka Nyabehu yamekuja Bunda Mjini. Katika mkataba wa ule mradi ilikuwa ni pamoja na kujengwa vituo. Hivi tunavyozungumza bado vituo havijajengwa Kata tu ya Gutagushigwamara hakuna kituo. Nyabeu yenye kiko kimoja, ukienda Kinyambwiga hakuna kituo, ukija Bunda *Store* huku hakuna kituo. Manyamanyama, Nyasura, Sazila hayo maeneo yote kama kungejengwa vituo tungeweza kupata maji katika Kata zote 14 kwa huo mradi uliochukua zaidi ya miaka 13. (Makof)

Sasa kwa mujibu wa ule mkataba ni lini sasa hivyo vituo vitakamilika ili wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda Mjini wasahau biashara ya kupata shida ya maji safi na salama? (Makof)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Lakini nataka nimuhakikishie sisi kama Wizara ya Maji tumefanya mageuzi makubwa sana, kuitia

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wizara yetu ya Maji na Rais wetu *support* kubwa ambayo anatupa ya kifedha. Tulikuwa na miradi kichefuchefu zaidi ya 177 asilimia nyingi tumekwisha ikamua. Sasa nataka nimpe mwaliko mahususi kabisa tarehe 7 Mheshimiwa Rais wetu mpenzi Mama Samia Suluhu Hassan atakuwepo Bunda. Naomba tujumuike ukaone kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na Wizara yetu ya Maji katika Jimbo lako. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Assa.

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Matatizo yaliyoko katika Jimbo la Mwibara na maeneo mengine ya Tanzania, yanafanana kabisa na matatizo yanayopatikana katika Jimbo la Kigoma Kaskazini. Ndani ya Jimbo la Kigoma Kaskazini tuna mradi wa Mkongoro I, ambaao umechukua muda mrefu na huu mradi unakwamisha adhima ya Mheshimiwa Rais ya kumtua ndoo mama kichwani.

Naomba kujua ni lini huu mradi utaukamilisha ili tuweze kuwasaidia mama zetu katika Jimbo la Kigoma Kaskazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge na nimeshafika katika Jimbo lake kiukweli unafanya kazi kubwa, unafanya kazi nzuri kama kijana. Sisi kama Wizara ya Maji tutaendelea kukupa ushirikiano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara yetu ya Maji tumesema miradi ambayo imetumia kwa muda mrefu mkakati wetu ni kuhakikisha tunaikamilisha. Nikuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge saa 7.00 tukutane tuone namna gani ya *ku-push* mradi ule ili tuweze kuukamilisha. Ahsante sana. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo sasa ni swali la Dkt. Christina Christopher Mnzava.

Na. 5

**Kupeleka Maji Kata za Imasela, Ilola, Lyamidati,
Lyabukande na Nyida -Wilaya ya Shinyanga**

MHE. JERRY W. SILAA K.n.y. MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA
aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapatia maji wananchi wa Vijiji vya Kata za Imasela, Ilola, Lyamidati, Lyabukande na Nyida ambao wapo ndani ya Kilometra 12 kutoka katika mtandao wa maji ya Ziwa Victoria?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa huduma ya maji katika Kata za Imasela, Ilola, Lyamidati, Lyabukande na Nyida zenye jumla ya vijiji 21 ni wastani wa asilimia 49.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Vijiji vya Kata za Imasela, Ilola, Lyamidati, Lyabukande na Nyida vilivyopo ndani ya Kilometra 12 vinapata huduma ya maji kutoka katika mtandao wa maji ya Ziwa Victoria, Serikali imepanga kupeleka maji Kata ya Imasela kuititia awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa Tinde - Shelui. Utekelezaji wa mradi huo, ulianza mwezi Agosti, 2021 na kwa sasa, umefikia asilimia 15. Natarajia kuwa ifikapo mwezi Agosti, 2022 mradi utakuwa umekamilika.

Aidha, Serikali imepanga kufanya usanifu wa mradi wa maji wa Kata za Ilola, Nyida na Lyamidati ambao utaanza

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mwishoni mwa mwezi Februari, 2022 na kukamilika mwezi Juni, 2022. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kata ya Lyabukande, usanifu umekamilika kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria katika vijiji vya Mwashagi na Buzinza. Ujenzi wa mradi katika Kijiji cha Mwashagi Kata ya Lyabukande utatekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha kwa kutumia fedha za UVICO – 19, ambapo Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 07 Januari, 2022 na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2022. Kwa upande wa Kijiji cha Buzinza, utekelezaji wa mradi utaingizwa katika bajeti ya 2022/2023.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jerry Silaa kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Christina.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali na niruhusu vile vile kumpongeza kidhati Mheshimiwa Jumaa Aweso Waziri wa Maji kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya katika kutekeleza miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi na shukurani hizi vile vile zimfikie Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumuamini kwenye Wizara hii. Ninaamini wale ambaao huwa wanapita pita kutoa zile *PhD* kama za Dkt. Musukuma punde tu watampa Udaktari wa Miradi ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu haya mazuri na kwa ahadi ya Serikali ya kufikia Mwezi Agosti, 2022 miradi hii itakamilika je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana na Mheshimiwa Mnzava kufanya ziara punde tu baada ya Bunge hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana kaka yangu Jerry Silaa kwa kazi kubwa ambayo anayoifanya, katika Jimbo lake la Ukonga kwa kweli anafanya kazi kubwa na nzuri sana na yenye kuonekana. Lakini kubwa kuhusu suala la kwenda katika Jimbo la Mkoa wa Shinyanga niko tayari baada ya Bunge hili. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Bilakwate.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa nafasi ambayo amekuwa akinipa kujadili miradi ya Wilaya ya Kyerwa.

Swali langu la nyongeza, tunao mradi wa vijiji 57 na mradi huu Mheshimiwa Waziri tumekubaliana unajengwa kwa awamu. Lakini kuna mradi unaotoka Kyerwa, Nyaruzumbula, Nyakatuntu mpaka Kamuli. Mradi huu umechukua muda mrefu ni lini mradi huu utanza? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote dhati ya moyo nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Kyerwa kwa kazi kubwa na nzuri, ambayo analifanya na amekuwa msombofu sana kuhusu suala zima la Jimbo lake liweze kupatiwa huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan sisi Wizara yetu anatupatia fedha kila mwezi kupitia Mfuko wa Maji na tumetengewa zaidi ya shilingi bilioni 459.2 kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji vijiji. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ahadi ambazo tuliziahidi kama Wizara ya Maji tutakwenda kuzitekeleza kwa sababu ya upatikanaji wa fedha ambazo tunapewa na Mheshimiwa Rais. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko swali fupi la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni dogo kweli na fupi. Sote tunakumbuka wakati wa bajeti hapa Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba ile Miji 26 ya Miradi ya (*India*) itatekelezeka ndani ya muda. Lakini leo wakati Mheshimiwa Mwanyika anauliza kutaka kujuu *status ambapo* tuna mradi huo wa kutoka Ronya kwenda Tarime Mjini. Tunataka kujuu *exactly* ni lini utakamilika huu mradi? Sio kwamba mtuambie mnasubiri kibali kutoka *Exim Bank* ni lini utakamilika? Maana yake wananchi wanategemea kupata huduma hii ya maji. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo fupi Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na najua dhati ya moyo namna gani wananchi wako wanataka huduma ya maji. Utekelezaji wa miradi ya maji lazima tukubali upitie taratibu ama michakato mbalimbali ambayo inahitajika. Michakato ya manunuzi sisi kama Wizara ya Maji tumekwishaikamilisha. Tunakamilisha taratibu za manunuzi lazima tupeleke katika *Exim Bank* ambao wanatupa kibali cha (*no objection*). Sisi kama Wizara ya Maji tumeshazungumza na wahusika kuna mambo machache ambayo wanayakamilisha na muda si mrefu tutapata kibali kile kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge Subira yavuta kheri na kheri itapatikana juu ya utekelezaji wa miradi ya maji. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mulugo nimekuona.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, afadhalii. Swali langu moja kwa Wizara ya Maji. Kampuni ya (*DDCA*) au Wakala wa Kuchimba Visima nchini Wilaya ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Songwe kuititia *TARURA* Songwe tumewalipa Shilingi milioni 158 tarehe 24 Novemba, 2021 kwa ajili ya kuchimba visima ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maji. Lakini mpaka leo Kampuni hiyo haijachimba visima na nimekuwa nikiwasiliana na *CEO* wa *DDCA* anakosa majibu na gari lipo lakini hawajaja bado kuchimba visima katika Wilaya ya Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri ni lini sasa gari hilo litakuja Wilaya ya Songwe kwa sababu Wilaya ya Songwe ni *scattered* na mvua zimeshaanza kunyesha na kuna baadhi ya maeneo mwezi huu njia ile itakuwa haipitiki kwa sababu ya mvua?

Lakini je, nilikuwa najaribu kumuomba Mheshimiwa Waziri atafute Kampuni nyingine tuweze kuchukua fedha *DDCA* tuweze kuchimba visima kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maji Songwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAJI: Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa wa Songwe kaka yangu Mulugo kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya katika Jimbo lako. Nataka nimuhakikishie nikiri Waheshimiwa Wabunge kama mnakumbuka katika Bunge la Bajeti, mlitoa changamoto juu ya utendaji katika suala zima la Wakala wetu wa Maji na Uchimbaji Visima na Mabwawa (*DDCA*). Tulikuwa na changamoto ya kiutendaji tumeshafanya mabadiliko hususani Mkurugenzi yule ambaye anasimamia Taasisi ile na muda mfupi mtaona mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Maji hatupo tayari kuona wananchi wa Songwe wanateseka ili hali fedha zimeshalipwa. Nikuombe Mheshimiwa Mbunge tukutane tufanye *alternative* ya haraka katika kuhakikisha visima vile vinachimbwa na wananchi wanufaike na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix Mbunge wa Buhigwe. (*Makofii*)

Na. 6

Kupanua Uwanja wa Ndege Kigoma - Buhigwe

MHE. KAVEJURU E. FELIX Aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanua Uwanja wa Ndege wa Kigoma ili Ndege kubwa ziweze kutua?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini ili niweze kumsaidia katika nafasi hii naomba nimuahidi yeye Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge pamoja na watanzania kwa ujumla kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa uaminifu na uadilifu kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Kigoma ni mionganini mwa Viwanja vya Ndege vinne (4) ambavyo ni Kigoma, Tabora, Sumbawanga na Shinyanga vinavyotarajiwa kujengwa na kukarabatiwa kwa Ufadhilli wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank - EIB*). Ambapo miradi mingine yote imekwishapata Makandarasi isipokuwa mradi wa upanuzi wa Kiwanja cha

Ndege cha Kigoma. Kwa sasa, taratibu za makubaliano ya Kimkataba tayari zimeshakamilika kati ya Serikali na Mfadhili huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kuwa na Mfadhili, kazi zingine ambazo ziko nje ya makubaliano zitatekelezwa na Serikali moja kwa moja. Aidha, Serikali itahusika na kazi ya urefushaji wa barabara ya kuruka na kutua Ndege kutoka mita 1,800 zilizopo kwa sasa hadi mita 3,100. Ambapo tayari Usanifu wa kina umefanyika kwa lengo la kuwezesha ndege kubwa kutua na kuruka bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kazi zinazofadhiliwa na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank - EIB*) katika mradi wa Kiwanja hiki cha Ndege, Serikali inasubiri idhini (*no objection*) kutoka kwa Mfadhili ili kukamilisha mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayetekeliza mradi huu. Aidha, kazi ambazo zinatarajiwu kufanywa kwa ufadhilli wa Benki hiyo ni Ujenzi wa Jengo jipya la Abiria, Jengo la Kuongozea Ndege, Upanuzi wa Maegesho ya Ndege, Usimikaji wa taa za kuongozea ndege pamoja na uzio wa usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali imejipanga kuanza upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma mara baada ya kumpata Mkandarasi atakayetekeliza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kavejuru Felix swali la nyongeza.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Pamoja na mikakati ambayo Serikali imeionyesha je, ni lini sasa ujenzi huo utaanza? (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(b) Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma una Wilaya tatu mpya ambazo ni Buhigwe, Kakonko na Uvinza. Wilaya hizi hazina viwanja vidogo nya ndege. Serikali ina mkakati gani? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GEOFREY G. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyezekiti, Mheshimiwa Kavejuru amekuwa anafuatilia sana suala la ujenzi wa kiwanja hiki, lakini naomba tu nimtoe wasiwasi kwamba kwa maelewano ambayo yanaendelea, tunategemea tarehe 28 mwezi huu wa Pili, kupata *Letter of No Objection* na miradi yote hii minne tunaamini itaanza kutekelezwa. Hilo ni jibu la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, jibu la pili kuhusu ujenzi wa viwanja nya ndege vidogo ama *air strip* katika Wilaya za Buhigwe, Kakonko na Uvinza, hili litategemea na upatikanaji wa fedha kadri itakavyoruhusu, basi hivyo viwanja vinaweza vikajengwa. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki.

Na. 7

**Barabara ya Manyoni East – Heka – Isseke – Sanza
hadi Dodoma**

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Manyoni East – Heka – Isseke - Sanza hadi Dodoma.

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Waziri.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG.
GEOFREY G. MSONGWE) alijibu: -**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Manyoni East – Heka – Isseke – Sanza – Chali – Igongo hadi Bihawana Junction Dodoma ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Barabara hii ina urefu wa kilometra 193 na katii ya hizo kilometra 124 ziko Mkoa wa Singida na kilometra 69 ziko Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali imekamilisha usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa daraja la Sanza lenye urefu wa mita 75 liliopo kwenye barabara hii. Kazi hii ilikamiliwa mwaka 2018. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha za kulijenga. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara hii zitafuata kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili kuhakikisha kuwa inaimarika na kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka huu wa fedha wa 2021/2022, jumla ya Shilingi milioni 1,513.284 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Chaya swalii la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na majibu ya Naibu Waziri ni kwamba tangu mwaka 2018 tayari upembuzi yakinifu ulishafanyika.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Swali la kwanza, ni lini sasa Serikali itamalizia kuwalipa fidia wale wananchi wa vijiji vya Ikasi, Sanza na Chicheho ambao wanadai takribani shilingi milioni 60 ili kupisha ujenzi wa lile daraja? (*Makofii*)

Swali la pili ni kwamba, barabara hii ya kutoka Manyoni - Heka - Sanza mpaka Dodoma inaunganisha Halmashauri Nne; Halmashauri ya Itigi, Halmashauri ya Manyoni, Halmashauri ya Bahi na Halmashauri ya Dodoma Mjini. Kwa mantiki hiyo, hii ni barabara muhimu sana kwa sababu inaleta watu kwenye Makao Makuu ya nchi: Je, Serikali haionti sasa ni muda muafaka kuhakikisha kwamba tunatafuta vyanzo vya fedha ili kufungua hii barabara kukuza Mji wa Dodoma? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GEOFFREY G. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Daraja la Sanza ambalo litakuwa na urefu wa barabara kilomita 14.5 pande zote mbili limeshafanyiwa usanifu na tunavyoongea hivi, kama Wizara tayari tulishapeleka maombi ya fedha Wizara ya Fedha ili tuweze kuwafidia wananchi wote ambao watapisha ujenzi wa barabara. Baada ya hapo, kama Mheshimiwa Mbunge alivyoushaza, tayari tumeshatenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ni muhimu kama alivyo sema, lakini haitapitika kama daraja lile halitajengwa. Kwa hiyo, Serikali iliona ni busara kwanza tujenge hilo daraja ili kuwe na mawasiliano ya moja kwa moja mwaka mzima. Ndiyo maana kama nilivyo sema, kwa umuhimu huo ambao unaunganisha Halmashauri nne alizozitaja, tunaamini baada ya kukamilika daraja usafiri utakuwa na uhakika na baadaye

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tutaanza kutafuta fedha kujenga kwa kiwango cha lami.
Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi kidogo kufuata Kanuni, maswali ya nyongeza angalau yawe yanafanana na maudhui ya swali la msingi ili Mawaziri waweze kujibu kwa uhakika zaidi.

Nimemwona Mheshimiwa Ndaisaba.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Changamoto iliyopo Manyoni Mashariki ni sawa na changamoto iliyopo kwenye Jimbo la Ngara ambapo Serikali ilituahidi miaka 15 iliyopita kutujengea barabara ya Murugarama, Rulenge na Rusahunga kilomita 85 kwa kiwango cha lami. Kwa masikitiko makubwa miaka 15 iliyopita hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua sasa: Ni lini; kwa maana ya dakika, saa, siku, mwezi na mwaka ambapo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itaanza kujenga barabara yetu kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri alikuja mwaka 2021, tukaahidi wananchi kwamba barabara hii inaenda kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Naomba niambiwe saa, siku, mwezi na mwaka ambapo barabara hii inaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Ah, Mheshimiwa Mbunge hilo ni swali kweli unauliza mpaka saa? Mheshimiwa Waziri majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GEOFREY G. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilitembelea Jimbo la Ngara na moja ya eneo ambalo tulilitembelea ni hii

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

barabara. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Ngara, pamoja na wananchi wa Ngara kwamba dhamira ya Serikali bado ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba bajeti tunayoendelea kuitekeleza tulitenga fedha. Kwa hiyo, mara fedha itakapopatikana, ujenzi wa barabara hii utaanza kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga na baadaye Mheshimiwa Kunambi nimekuona.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninashukuru kwa kupewa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Naomba kuuliza, barabara ya kutoka Makete kwenda Mbeya takribani kilomita 97 ni barabara ambayo ilipata kibali cha Mheshimiwa Rais katika barabara 16 ambazo tulisomewa kwenye bajeti. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais ameongeza kutoka kilomita 25 kwenda kilomita 36.5 za kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini hadi dakika hii ninapozungumza ni kwamba bado tumbaki kwenye mchakato wa *tendering* toka mwezi wa Tisa.

Je, ni lini mchakato wa tenda utakuwa umeisha na barabara hii iweze kuanza kujengwa kwa sababu hili ndilo geti la uchumi kwa Wilaya ya Makete lakini pia kwa Mkoa wa Mbeya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GEOFFREY G. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru kwa kuipongeza Serikali na kwamba barabara yake ni kati ya barabara zilizopata vibali. Hata hivyo nataka nimhakikishie

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Sanga Mbunge wa Makete, kwa kuwa barabara ilishapata kibali cha Mheshimiwa Rais kwamba iendelee kujengwa, taratibu za manunuzi haziwezi zikakiukwa. Kwa hiyo, kama kuna changamoto ambayo ipo, labda Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa naomba tukutane tuone kuna tatizo gani? Ila ni kweli kwamba ikishapata kibali inatakiwa ujenzi uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba baada ya kikao hiki tuone kama kuna changamoto yoyote tofauti na taratibu za kawaida ili kama Wizara tuweze kuzitatua. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Morogoro – Njombe – Boda, umuhimu wake inaunganisha Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na ni barabara inayotoa *alternative*, yaani ni barabara mbadala kwa Mikoa ya Mbeya - Iringa - Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu dogo la nyongeza ni kwamba, barabara hii ina urefu wa kilomita takribani 222 na kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha zimetengwa fedha ili ujenzi uanze walau kilomita 50; na taarifa nilizonazo, imeshapata kibali: Ni lini sasa Wizara itaanza utekelezaji wa barabara hii? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GEOFREY G. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema, taratibu za manunuzi zinaendelea na mara zitakapopatikana, basi kilomita hizo zitaanza kujengwa. Siwezi nikasema ni lini na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tarehe gani, kwa sababu taratibu za manunuzi zina utaratibu wake, zinaweza zikachukua wiki au mwezi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itaanza kujengwa katika kipindi hiki cha bajeti. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 8

Umuhimu wa Kutathmini Ukadiriaji wa Kodi

MHE. AGNESTA L. KAIZA aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukutana na Wafanyabiashara na kutafuta namna bora ya kuwa na utaratibu wa ukadiriaji kodi wenyewe usawa na unaozingatia mabadiliko ya biashara ili kulinda mitaji ya wafanyabiashara wa ndani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa idhini yako naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Rahim, ambaye ametujalia afya na uzima. Jambo la pili, nimshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Tatu ninaomba niwashukuru sana Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wao mkubwa kwangu, dua na sala zao kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukadiriaji wa kodi hufanyika kwa mlipakodi kuandaa taarifa za biashara yake na mwisho

wa mwaka kufanya makadirio ya kodi kulingana na taarifa hizo. Kwa msingi huo, mlipakodi hufanya makadirio mwenyewe (*Self-Assessment*). Kazi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ni kuhakiki usahihi wa makadirio aliyofanya mlipakodi endapo yamefuata matakwa ya sheria. Kwa hiyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania hukutana na walipakodi mara kwa mara kwenye michakato ya ukadiriaji wa kodi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa wafanyabiashara kujikadiria kodi wenyewe ni utaratibu unaotumika na kukubalika duniani kote. Utaratibu huu umewekwa kwa madhumuni ya kukuza mwamko wa ulipaji kodi kwa hiari (*Voluntary Tax Compliance*), kurahisisha ukusanyaji kodi na kupunguza gharama za ukadiriaji. Hata hivyo, biashara ambazo hazifuati misingi ya utunzaji kumbukumbu hulazimika kuingizwa kwenye utaratibu wa ukadiriaji kulingana na mauzo (*Presumptive Tax System*) ambapo *TRA* hutoa makadirio ya kodi kulingana na mauzo ya biashara husika katika kipindi cha mwaka. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnesta Lambert swalii la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Wafanyabiashara wengi wenye mitaji midogo hawana elimu ya kutosha kuhusiana na suala zima la kufanya makadirio yao wenyewe ya kulipa kodi. Jambo hili limepelekea wafanyabiashara hawa mara nyingi kuajiri wataalam wa kuja kuwasaidia jambo ambalo hupelekea wao kutozwa fedha nyingi kuanzia shilingi laki tano, milioni moja na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa ni changamoto sana kwa wafanyabiashara na mwisho wa siku wafanyabiashara wengi wameshindwa kuendelea na biashara kwa maana wamekata tamaa kwa kuwa mwisho

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wa siku wanajikuta hawapati chochote, kila wanachokifanya kinaishia katika kulipa wataalam.

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kutoa elimu sahihi kwa wafanyabiashara hawa hususan wafanyabiashara wa vijiji ambao kimsingi elimu kwao haipo kabisa? Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, wafanyabiashara hawa wenye mitaji midogo walikuwa wamewekewa utaratibu maalum wa makadirio ya shilingi 20,000/= kwa mwaka, lakini mpaka sasa ninapoongea utaratibu huu upo kimya kabisa, ni kama haupo: Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na utaratibu huu ambao upo kimya kwa wafanyabiashara hawa ikiwa ni sambamba na kwa wafanyabiashara wenye maduka siyo tu kwa machinga. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba nimpongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Agnesta kwa namna anavyotetea Wafanyabiashara wadogo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la taaluma, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na hata wakubwa kupitia runinga, redio, na matamasha. Inawezekana baadhi ya vijiji elimu hiyo haijawafikia. Tutachukua ushauri huu kushuka chini vijiji kabisa kwa ajili ya kupeleka elimu ya kulipa kodi hasa kwa hiari. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la pili; kuhusu utaratibu wa wafanyabiashara wadogo kulipa ada ya shilingi 20,000/= kwa mwaka bado upo na unaendelea kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo kupitia vitambulisho vya Machinga. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya Fedha, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni aulize swali lake.

Na. 9

Utoaji wa *Tax Clearance* kwa Biashara za Maduka

MHE. TARIMBA G. ABBAs aliuliza: -

Utoaji wa leseni za biashara kwa biashara ndogo za maduka katika Manispaa ya Kinondoni umekuwa na changamoto kutokana na wafanyabiashara hao kutokuwa na *Tax Clearance* kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*).

Je, ni kwa nini Serikali Isiiagize *TRA* kwenda mitaani na kubaini biashara hizo na kuzisajili kwa lengo la kurahisisha utoaji wa *Tax Clearance* ili leseni ziweze kutolewa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganii mwa changamoto zinazopelekea wafanyabiashara kutopatiwa *Tax Clearance* ambalo ni takwa la kupatiwa leseni ya biashara, ni pamoja na wafanyabiashara hao kutosajiliwa na kupatiwa namba ya utambulisho wa mlipakodi (*TIN Number*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto hii kwa wafanyabiashara, Serikali imeongeza kasi ya zoezi la usajili wa walipakodi katika jiji la Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea na kampeni ya mlango kwa mlango ili kutatua changamoto zinazowakabili walipakodi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kodi, kuwatambua walipakodi wapya na kuwasajili. Lengo la kampeni hii ni kurahisisha zoezi la usajili wa walipakodi kwa kuwasogezea karibu huduma hii wafanyabiashara wote nchini, kwa kuwafuata katika maeneo yao ya biashara badala ya kuwasubiria waje katika Ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili maalum limeanza mwezi Agosti, 2021 katika mikoa yote ya kikodi katika Jiji la Dar es Salaam ikiwemo Manispaa ya Kinondoni na litaendelea nchi nzima. Ni matumaini ya Serikali kuwa zoezi hili litaongeza idadi ya walipakodi waliosajiliwa na hivyo kurahisisha upatikanaji wa *tax clearance* ili leseni za biashara ziweze kutolewa kwa uharaka zaidi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gulam Abbas, swali la nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jitihada za kunijibu ingawa swali langu la msingi niliuliza ni lini sasa Serikali itakwenda mitaani, itashuka chini kwa maana ya *TRA* kuweza kuwabaini wafanyabiashara hawa waweze kuandikishwa na hatimaye waweze kupata *tax clearance*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu tunaona kwamba, Serikali inasema kuna kampeni ya mlango kwa mlango, nataka nikiri, sijaiona kampeni hiyo na kwa hali hiyo kama utaratibu huo upo maana yake ni kwamba, utachelewesha sana kuweza kulifanya zoezi hili:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu; kwa kuwa, Serikali imeweza kufanikisha kuwepo kwa Maafisa kwenye kila kata, kwa mfano Maafisa wa Elimu, Maafisa Afya, Maafisa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kilimo, na kadhalika; ni kwa nini sasa Serikali isifikirie kuwa na Maafisa Kodi kwenye kila kata ili waweze kufanya kazi ambayo ni ya kuwafikia kwa urahisi wafanyabiashara ambao kila siku wanalamikia masuala ya *tax clearance* na *license*? Kule Kinondoni shida ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı langu la pili; ili kuweza kuwabaini wafanyabiashara hasa hawa wadogowadogo katika maeneo yetu, je, Serikali haioni busara kama inaweza ikaanzisha madaftari katika kila mtaa kuweza kuwabaini wafanyabiashara ndogondogo ili matatizo yao ya elimu ya ulipaji wa Kodi na masuala mengine yakatatuliwa kwa urahisi, badala ya kuzungumzia elimu ambayo inatolewa na mamlaka kuitia kwenye ofisi za Kodi kiasi kwamba, si rahisi jambo hilo kuweza kutekelezeka zaidi ya nadharia? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kwa namna anavyowapigania na kuleta maendeleo katika Jimbo lake la Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Abbas, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la kushuka chini ni kama ambavyo tumezungumza katika swalı la mwanzo la Mheshimiwa Agnesta. Serikali yetu iko tayari kushuka chini kwenda hadi Serikali za Mitaa kwa ajili ya ukusanyaji wa Kodi, lakini la kuanzisha maafisa ndani ya Serikali za Mitaa, hili tutachukua kama ni wazo na ushauri na tutautekeleza baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Abbas kwamba, kampeni ya mlango kwa mlango ipo na pengine tu kutokana na majuku yake mengi hajashuhudia. Hii ni kwa sababu, tayari mpaka kufikia tarehe

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

31 mwezi jana, basi walipakodi 432,323 ndani ya Kinondoni peke yake tumewasajili tayari na wafanyabiashara kati ya hao ni 171,973 kwa hiyo, suala hili la mlango kwa mlango liko Mheshimiwa Abbas. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Tunaendelea na Wizara ya Afya, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 10

Ujenzi wa Wodi za Wagonjwa wa Matatizo ya Ubongo na Akili Dar es Salaam

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Wodi za Wagonjwa wenye matatizo ya Ubongo na Akili katika Hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini vilevile kumshukuru Rais wetu kwa kuendelea kutuamini mimi na Mheshimiwa Ummy Ali Mwalimu kusimamia Wizara ya Afya kwa niaba yake Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Temeke ipo katika mchakato wa kukarabati jengo lililokuwa likitumika kwa wagonjwa wa kisukari ili liweze kutumika kwa ajili ya kulaza wagonjwa wa akili. Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala imetenga kiasi cha shilingi milioni mia mbili

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya wagonjwa wa akili. Pia, Hospitali ya Rufaa ya Amana kwa kuwa ujenzi huo upo kwenye mpango mkakati wa miaka mitano wameelekezwa kutenga bajeti ya ujenzi wa jengo la afya ya akili katika bajeti ya mwaka 2022/2023. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swalii la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa kwa sasa wagonjwa wote wa akili katika Hospitali za Temeke, Mwananyamala na Amana, wanapelekwa katika Hospitali ya Muhimbili, lakini jengo hilo la wagonjwa wa akili la Hospitali ya Muhimbili halijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu kiasi kwamba, mwananchi wa kawaida kuingia kwenye ile wodi unaogopa. Sasa napenda niilizie Serikali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati jengo la wagonjwa wa akili katika Hospitali ya Muhimbili, ili Madaktari wetu waweze kufanya kazi zao katika mazingira mazuri na wagonjwa waishi katika mazingira mazuri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa, takwimu za Shirika la Afya Duniani (*WHO*) zinaonesha kwamba, kuanzia mwaka 2020 kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa akili duniani na hasa vijana kuanzia miaka 15 mpaka miaka 35 na hiyo inatokana na matatizo na changamoto mbalimbali za kimaisha. Haya yameanza kujitokeza katika nchi yetu ya Tanzania, watu wameanza kuuana ovyo na matendo ambayo sio ya kibinadamu yanatendeka sana, tunapata hizo taarifa. Je, Serikali haioni haja sasa ya kujenga hospitali maalum ya wagonjwa wa akili badala ya kuwa Mirembe, Dodoma peke yake? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mbunge kwa ufuatiliaji mzuri sana anaoufanya kwa kufuatilia masuala ya afya ya watu wanaoishi kwenye Mkoa wa Dar-es-Salaam, tunampongeza sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema kwamba, kweli jengo lile liko chakavu pale Muhimbili, lakini kwa mwaka huu tu, hii miezi miwili iliyopita, hospitali ya Muhimbili Rais wetu amepeleka bilioni 16 pale, lakini ilitengwa zaidi zaidi ya milioni 400 kwa ajili ya kukarabati jengo lile, lakini kwa sababu ya matatizo ya *corona* na kulikuwa na umuhimu wa kuhamkisha baadhi ya *expenses* zilizoongezeka wangebeba wananchi wenyewe ingeleta shida, fedha zile zilielekezwa upande huu, lakini ameshatoa maelekezo Waziri wa Afya juzi alivyotembelea Muhimbili na sasa hiyo kazi inaenda kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Swali lake la pili amezungumzia kwamba, kuna matatizo ya akili yameongezeka duniani, lakini vilevile hapa nchini kwetu Tanzania. Ni kweli, yameongezeka, suala sio kuongeza idadi ya hospitali, lakini ni kuangalia visababishi ambavyo vinasababisha watu kupata matatizo hayo viweze kutatuliwa. Vilevile sio tu kujenga hospitali maalum kwa ajili ya hiyo, lakini ni ku-*integrate* hizi huduma kwenye huduma nyingine mpaka kushuka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu ameshaelekeza kwamba, hospitali zote zianze na nilanza na Kigoma kama uliangalia kwenye vyombo vy ya habari, kulikuwa na wataalam wa afya ya akili na wale wataalam wa afya ya akili tukaanza kuelekeza kwamba, waanze sasa kutengewa bajeti na zile ofisi zao zipewe bajeti ya kutosha ili wawewe kufanya kazi zao na kushuka chini mpaka kwenye vituo vy afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata unapoona *CT-Scan* zimesambazwa kwenye hospitali zote za mkoa, wakati mwininge wagonjwa wa akili wamekuwa wakitibiwa kwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuangalia dalili zao tu, lakini sasa tunataka kwenda kuwaangalia kabisa, kwa sababu wanaweza wote kuonesha dalili zinazofanana, lakini visababishi vikawa tofauti. Kwa hiyo, sasa tunaenda kwenye *level/ya kupiga CT scanza* ubongo ili kila mmoja aweze kutibiwa kwa namna ambavyo ana tatizo lake. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la afya ya akili hata katika Mkoa wetu wa Iringa limekuwa kubwa sana na changamoto kubwa kabisa ya tatizo hili ni kwamba, bei ya dawa iko juu sana, sana. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba, dawa zinakuwa na bei ndogo au kuondoa kabisa, ili waweze kupatiwa bure kama yalivyo magonjwa mengine?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba nijibu swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwanza dawa za wagonjwa wa akili zinatolewa bure na tayari Serikali imeshapeleka kwenye maeneo yote watu wa kufanya hivyo. Kama kuna mahali wanawauzia kwa Mkoa wa Iringa, nitalifanya kazi ili kuona namna ya kufanya. Nalipokea ili tuweze kulifanya kazi. Wote tutaona kwamba Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ameshaunda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, mojawapo ya kazi ni kuhakikisha, ile Wizara itakaposimama kwenye eneo lake tutapunguza sana mambo yanayosababisha yanayoongeza idadi ya watu wenye matatizo ya akili kwenye jamii.

Kwa hiyo, kikweli nachukua wazo la Mheshimiwa la dawa, lakini tutaenda kulifua tilia zaidi na kwenda Iringa kuimarisha zaidi hicho kitengo ambacho umekizungumzia hasa kwenye eneo la dawa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha nimekuona.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikiri kabisa kwamba, Wizara ya Afya kwa kweli, kwa upande wetu Jimbo la Hai wanatutendea haki, lakini naomba niulize swali. Hospitali yetu ya Wilaya ya Hai ni chakavu sana na watumishi wanapata tabu kweli kutoa huduma pale. *Walk ways* zimekuwa chakavu, hatuna jengo la mama na mtoto, hatuna jengo la *pharmacy*, kiufupi hospitali hii ni chakavu na Naibu Waziri anaifahamu vizuri. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati katika hospitali yetu ya Wilaya ya Hai?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Hai kwa jinsi ambavyo anapambana na matatizo ya watu wa Hai. Kwenye hospitali hiyo ya Hai Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan amepeleka milioni 220, amepeleka 300, akapeleka tena milioni 90 kwa ajili ya kujenga nyumba ya watumishi, hata hivyo, nakubaliana na ye ye kwamba, kwa kweli hospitali hiyo ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipita mimi na ye ye na kikubwa tuliongea na *DMO* pale kwamba, sasa waanze kuweka kwenye mchakato wa bajeti ya mwaka huu ili itakapofika fedha zimepatikana basi liweze kutekelezeka kulingana na taratibu za fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema nimekuona kule mwisho.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama ilivyoelezwa hapo awali kwamba, kumekuwa na ongezeko la matatizo ya akili na tunafahamu ongezeko la matatizo ya akili ni pamoja na kukosekana kwa watu wa ushauri na unasihi. Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha inaongeza Maafisa Ustawi wa Jamii mpaka ngazi ya kata? Ahsante.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Tunachukua hilo wazo, lakini katika sehemu nyingi kuna Maafisa Ustawi wa Jamii, bahati mbaya tu tukienda kwenye wilaya zetu wamepewa kufanya kazi nyingine, unakuta wengine ni Watendaji wa Vijiji au wengine wanafanya shughuli nyingine ambazo sio za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kikubwa kwanza tutaenda kusimamia waliopo kwanza wafanye kazi ambayo walitakiwa kuifanya na wawezeshwe kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa sababu tumefika kwenye *level* ya mkoa kupeleka wataalam hawa wanaoshughulikia masuala ya akili, basi tutashusha kwenye wilaya ikiwezekana kwenye vituo vyta afya jinsi bajeti itakavyoruhusu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara hiyo ya Afya. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini.

Na. 11

Upungufu wa Madaktari Bingwa na Vifaa Tiba

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA Aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya upungufu wa Madaktari Bingwa na vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete Mkoani Tabora?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA Alijibu:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa Kitete ina Madaktari Bingwa watatu wanaotoa huduma ya wanawake na watoto. Pia, Serikali imetoa ufadhili wa masomo kwa Madaktari sita wa hospitali hii ambao wanaseomea fani mbalimbali za kibingwa; fani hizo ni Wanawake na Afya ya Uzazi mmoja, Masikio, Pua na Koo mmoja, Magonjwa ya Ndani wawili, Huduma za Dharura mmoja na Mionzi (Radiolojia) mmoja. Madaktari hao wanatarajiwa kuhitimu mwaka wa masomo 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa jumla ya Shilingi Billioni 10.5 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (*ICU*) pamoja na vifaa vyake, jengo la huduma ya mama na mtoto, jengo la dharura (*EMD*) pamoja na vifaa vyake na ununuzi wa *CT-Scan* pamoja na jengo lake ambapo shughuli hizo zote zimeanza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakasaka swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Kitete, kama neno rufaa linavyoonesha, ndio hospitali tegemezi kwa Mkoa wa Tabora. Hospitali ile inahitaji Madaktari Bingwa wasiopungua nane na kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri kwamba, kuna Madaktari watatu, ingawa mimi nafahamu kuna Madaktari Bingwa wawili yani kama ilivyo jibu lake la msingi, kwa watoto na akinamama; hatuna Madaktari wa upasuaji, hatuna Madaktari wa mifupa, hata physician hawapo kwa hiyo, hatuna Madaktari wengi na hii ni hospitali ya rufaa. Niseme namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kutupa shilingi hizo bilioni 10.5 kwa

ajili ya ujenzi wa majengo ya dharura pamoja na majengo ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza; je, baada ya Mheshimiwa Rais kutoa fedha zote hizo na majengo tayari yamekamilika, hayana Madaktari Bingwa kwa muda mrefu, Wizara ya Afya hamuoni mnaanza kudidimiza hata juhudini za Mheshimiwa Rais kwa kutoleta madaktari bingwa katika majengo hayo mazuri ambayo yanajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa, sehemu zingine kuna Madaktari Bingwa wengi sana, ikiwemo Dar-es-Salaam. Na kwa kuwa, Madaktari wengi hawaendi kwenye mikoa mingine kama Tabora kwa sababu ya vivutio. Je, Wizara imejipangaje kuweka vivutio kwa madaktari hawa bingwa ili waweze kuvutiwa kufanya kazi sehemu kama Tabora Mjini? ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijiblu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja amesema Madaktari ni wawili sio watatu; mimi ninachoweza kumwambia mpaka mwisho wa mwaka huu maana yake wanaenda kuongezeka Madaktari sita. Wanapoongezeka maana yake watakuwa, tulitegemea wawe tisa, lakini maana yake unasema watakuwa nane, lakini nataka kukuhakikisha watakuwa tisa mpaka tunapofika mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *specifically* ametaja baadhi ya magonjwa na matatizo yanayowasumbua zaidi kwenye eneo lao; tayari Waziri wa Afya ameshaelekeza upembuzi yakinifu ufanyike nchi nzima kujua maeneo yenyewe Madaktari wengi kuliko mahitaji halisi, ili kuweza kuwapeleka katika yale maeneo ya pembezoni ambayo yana uhitaji zaidi.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amezungumzia suala zima la kwamba, la watumishi kwa ujumla kwamba, majengo yanakwenda kwisha na wakati mwingine majengo yanakuwa mazuri, lakini ndani yake hakuna watumishi wa kufanya kazi hiyo; lakini nimwombe Mheshimiwa Mbunge suala la watumishi wa afya kuwa wachache sio suala tu la Tabora peke yake ni suala la nchi nzima na ni tatizo ambalo hata wanapokwenda shulen i kuwa *recruited* wanakuwa vilevile wachache, kwa hiyo kwenye soko kuwapata aina ya kada unayotaka wakati mwingine ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba tumechukua; na hata wakati fedha hizi shilingi trillion 1.3 ambazo Mheshimiwa Rais wetu ameipa Sekta ya Afya shilingi bilioni 495, alielekeza kwamba wakati ujenzi huu unaendelea, vile vile tukae na TAMISEMI na kwa wakati huo huo tukae na Wizara ya Utumishi kujipanga kuhakikisha majengo yanapoisha na ujenzi huo unapoisha, watumishi wanapatikana wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mwakasaka usiogope jinsi fedha na ikama inavyotoka. Tutahakikisha kila mahali kunakuwepo na watumishi wanaoweza kutoa huduma. Pia tunapunguza hilo tatizo kwa kuhakikisha vilevile madaktari bingwa walioko Dar es Salaam na mikoani wanaweza wakachukua wale wagonjwa wanaotakiwa kupelekwa rufaa Dar es Salaam au kwingine au kuletwa Benjamin, wakawafuata huko huko Kitete na kutibiwa huko huko ili kupunguza wananchi kuja Benjamin au kwenda Dar es Salaam. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Humphrey Polepole nimekuona.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani; na ni lini itaanza kuwezesha majaribio ya kitabibu au kwa Kiingereza wanaita *clinical trials* kwa bidhaa za mimea dawa ambazo zimesajiliwa na Baraza la Tiba Asili na mbadala na tayari

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

zinatumika kwa uhiyari wa wagonjwa kama *over the counter drugs* na zimeonyesha ufanisi mkubwa katika kutibu magonjwa mbalimbali yakiwemo ya mfumo wa upumuaji? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Labda nimwambie tu siyo kwamba ni lini itaenda kuanza, imekuwa ikifanya hivyo; na taasisi yetu ya *NIMR* na kushirikiana na wadau mbalimbali wamekuwa wakifanya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakumbuka kwenye fedha hizi ambazo zimetoka, shilingi trilioni 1.3, katika fedha hizo, shilingi billioni 6.1 zilitengwa kwa ajili ya eneo hilo la tafiti ikiwepo na suala la tiba asili. Kama mnakumbuka hapa Bungeni, niliwahi kusema kwamba kuna kipindi Mheshimiwa Rais wetu alipeleka shilingi billioni 1.2 pale *NIMR* kwa ajili ya kufanya mambo kama hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaulizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Rais wetu ameielekeza Wizara kwamba tuwekeze nguvu nydingi sana kwenye eneo hili la kufanya tafiti za madawa yetu ya asili kwa sababu yametusaidia sana kipindi kile ambapo tunapitia wakati mgumu kwenye *Corona* wakati hakuna anayejua suluhu ni nini kwenye tatizo hili. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Massay swalii la mwisho kwa Wizara hii.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia shilingi 1,500,000,000 tukajenga Hospitali ya Halmashauri. Sasa hospitali hii inafanya *clinic* ya watoto pake yake, haina vifaa tiba na hasa madaktari bingwa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta vifaa tiba ili hospitali ile ifanye kazi kama ilivyokusudiwa na Serikali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake mzuri wa masuala ya wilaya yake. Labda nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala siyo fedha za kununua bidhaa hizo, tayari Rais wetu ametoa fedha na sasa ni mchakato wa manunuzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, nikimaliza muda wa maswali njoo tukae pamoja ili ueleze *specifically* na tuwasiliane na *DMO* wako ili aweze kutuletea *list specifically* kinachotakiwa ili kiweze kwenda kununuliwa na kufanyika haraka ili upate huduma hiyo. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 12

Uelewa Kuhusu Uvuvi Haramu

MHE. MARYAM AZAN MWINYI aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia wavuvi elimu ya uelewa kuhusu madhara ya uvuvi haramu ili wasifanye aina hiyo ya uvuvi na kuharibu mazingira ya maziwa na bahari nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ya kujibu maswali, lakini kwanza naomba nami nimshukuru Mwenyezi Mungu; na pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini katika Wizara hii kwa nafasi hii ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya shukrani, naomba sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni muhimu sana kuwapatia wavuvi elimu kuhusu madhara ya uvuvi haramu ili wasifanye uvuvi haramu na tuweze kullinda rasilimali za uvuvi nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, Serikali imekuwa ikitoa elimu hiyo kupitia vipindi vya redio, runinga, mikutano, vipeperushi, semina na maonesho mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wataalam wa Wizara wamekuwa wakitoa elimu kwa kuwafikia wavuvi na wadau wengine moja kwa moja katika maeneo yao ambapo kwa mwaka 2021/2022 mikoa ambayo tayari imefikiwa ni mikoa ya Tanga, Pwani, Mwanza, Mara, Kagera na Katavi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maryam Azan, swali la nyongeza

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa vile Serikali imetoe majibu mazuri sana, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, Serikali imefanya tathmini katika elimu inayotoa, kama kusaidia kupunguza uvuvi huu haramu ambao bado tunauona unaendelea?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Maryam Azan Mwinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wote tumekuwa tukifanya tathmini

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tupunguze mazungumzo. Tuzungumze taratibu, tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati wote tumekuwa tukifanya tathmini na ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba pamoja na elimu tunayoitoa, bado tatizo la uvuvi haramu liko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Serikali tumekubaliana; la kwanza, elimu ni jambo endelevu, kwa hiyo, tutaendelea nalo. La pili, ni kupanua wigo na kufanya ushirikishaji zaidi ili kusudi tuweze kupambana na vita hii ya uvuvi haramu kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie ya kwamba wavuvi walio wengi wanaelewa sana ya kwamba hiki ni sahihi na kipi kisicho sahihi. Tunazo changamoto za msingi sana ambazo zinawapelekea wakati mwingine baadhi yao; aidha kwa makusudi au kwa au kwa bahati mbaya wanaingia katika vitendo hivi haramu. Miongoni mwa changamoto hizo ni ongezeko la mahitaji ya hizi rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali tunafanya tathmini na tunaendeleza mikakati ya kuhakikisha tunafanya uendelevu wa rasilimali zetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malembeka na Mheshimiwa Aida, nimewaona

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameelezea jinsi gani walivyojipanga kutoa elimu ya kuondoa madhara ya uvuvi haramu; na mara nyingi uvuvi haramu hufanyika kwa vifaa duni na ambavyo siyo sahihi; na vifaa sahihi hupatikana kwa gharama kubwa; na wengi wanaofanya uvuvi haramu ni kwa sababu hawana vifaa vile:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua: Je, Serikali ina mpango gani ili kuinua kundi hili la wavuvi wadogo wadogo kiuchumi hasa katika Pwani yetu ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Angelina Malembeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana kwa kuwa amekuwa kila mara mstari wa mbele kwenye kuwasemea wavuvi hasa wavuvi wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, ni kwamba mkakati wetu ni kuendelea kurekebisha sheria zetu na kuziboresha. Hili ni jambo la kwanza ili kusudi ziweze kuendana na wakati, maana wavuvi wamekuwa kila mara wanagundua zana mpya, zana ambazo labda wakati mwingine kwa upande wa sheria zetu tunakuwa nyuma ya teknolojia hizi ambazo wavuvi wamezigundua. Kwa hiyo, huu ni mkakati wetu wa kuhakikisha tunakwenda nao sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kurekebisha katika masuala ya kikodi. Tumekuwa tukifanya hivyo kila mara ili zana zetu ziweze kukidhi haja ya wavuvi kwa maana ya bei; na tatu ni mkakati wetu wa kuunda vikundi vyta ushirika wa wavuvi na waweze kupata mikopo iliyo na riba nafuu kuitia

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Benki yetu ya Kilimo na hatimaye kuweza kuwasaidia kwenye kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tunayo dhana pana sasa ya uchumi wa *blue* ambayo tumedhamiria, Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba tunahamasisha na kutangaza dhana hii ambapo katika ukanda wote mathalan wa bahari ya hindi tuweze kutumia ipasavyo rasilimali zote zinazopatikana ili kuweza kuwafanya wavuvi wetu wawe na kipato kinachotosheleza kwa ajili ya kaya kwa maana ya familia zao na kuweza kuwa na mchango mpanga kwenye pato la Taifa letu.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa muwe watulivu wakati Waziri anajibu maswali angalau tusikie; na Waheshimiwa Mawaziri naomba mijibu maswali kwa ufupi. Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wizara tayari imeshaanza utaratibu wa kutoa elimu ya huo uvuvi unaoitwa haramu, mionganoni mwa wilaya zilizoathirika ni pamoja na Wilaya ya Nkansi ambao walichomewa nyavyo zao kwamba wanavua uvuvi haramu, lakini Serikali haijawahi kuwapatia mbadala wa nyavyo zinazoitwa halali. Leo wamejikongoja wachache wameendelea na uvuvi, wanavamiwa na watu kutoka Kongo na Burundi. Wajibu wa Wizara ni_kuwalinda wavuvi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, mna mkakati gani wa haraka wa kuwasaidia wavuvi hawa ambao wamevamiwa na vifaa vyao bado viko Kongo na Burundi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkansi, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jinai na kwa hiyo, litashughulikiwa katika utaratibu wa kijinai. Naomba kwa kuwa ni jambo mahususi, tuweze kushughulika nalo katika utaratibu wake. Hapa umetaja nchi ambazo ni majirani zetu. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba ni jambo mtambuka. Hapa umetaja jambo ambalo linawenza kushughulikiwa pia na Wizara, sisi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya na kwa sababu linahusisha nchi nyingine na Wizara ya Mambo ya Nchi na Nje na wengine tunaohusika katika masuala ya ulinzi na usalama wa Taifa letu. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Swali la mwisho kwa Wizara hiyo, nimemwona Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa uvuvi haramu umeathiri sana mapato hasa kwenye mabwawa mengi, pamoja na Bwawa la Mtera ambapo Halmashauri ya Iringa Vijijini imekuwa ikipata mapato yake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza mabwawa yaye mashamba darasa kwenye Halmashauri nyindi pamoja na Jimbo la Kalenga ili tuweze sasa kufundisha vijana wengi pamoja na akinamama na akinababa waanze kutegemea uchumi wa kufuga samaki kuititia haya mabwawa ambayo yatakuwa ni mashamba darasa? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mkakati wetu. Katika bajeti ya mwaka huu 2021/2022 kuititia mradi wa *AFDP* kwa maana ya *Agricultural Fisheries Development Program II*, tumetenga pesa kwa ajili ya kuweza kutengeneza

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mashamba darasa ya ufugaji wa Samaki. Hapa walengwa ni makundi ya vijana na akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkaribishe Mheshimiwa Kiswaga ili tuweze kushirikiana katika hatua hii. Yawezekana Wilaya ya Iringa Vijijiini kwa maana ya Jimbo lake likawa ni sehemu ya wanufaika. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Nafikiri masuala ya uvuvi na masuala ya ufugaji ni muhimu. Naamini Serikali itazingatia na kama mlivyoahidi, mtatekeleza kwa sababu naona Wabunge wameyasimamia sana haya masuala ya uvuvi.

Tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 13

Ajira Kupitia Tasnia ya Sanaa

MHE. SYLVIA F. SIGULA aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kutoa ajira rasmi na zisizo rasmi kupitia tasnia ya Sanaa?

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu katika Wizara hii mpya ya Utamaduni Sanaa na Michezo, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema na mjawa wa kadiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kwa mara nydingine na kunitfea katika Wizara hii. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Rais kwamba Wizara yetu hii pamoja na watendaji wa Wizara tutajipanga kweli kweli ili

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

matamanio yake aliyokusudia katika Wizara hii yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijibu swalii la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, kwanza kwa kutambua mchango wake kwa vijana. Amekuwa na mchango mzuri kwa vijana, nasi kama Wizara tunampongeza sana kwa kuwasemea vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kutambua kwamba swalii lake ni la msingi na la muhimu sana, ili kuwavutia wadau hasa vijana kujajiri katika Sekta ya Sanaa, mpango wa Serikali ni kuendelea kuboresha mazingira ya kazi za sanaa kwa kufanya mambo kadhaa. Moja ya mambo makubwa ambayo tunakwenda kuyafanya ni:-

Kwanza, ni kuhakikisha vifaa na vitendea kazi vya sanaa vinapatikana kwa bei nafuu kwa kufanya mapitio kwenye kodi za vifaa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tutakwendu kuititia upya tozo kwenye Kanuni za *BASATA*, *COSOTA* na Bodi ya Filamu Tanzania ili ziwe rafiki kwa walipaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tutakwenda kuanzisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya usajili, ambayo mingine tunayo lakini tutakwenda kubuni na kuendeleza mingine ya maombi ya vibali na leseni pamoja na mfumo rasmi wa ukusanyaji mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, tutakwenda kujenga miundombinu ya sanaa kama vile *Arts Arena*, *National Art Gallery* na *One Stop Center*, ambayo tayari tunayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunakwenda kuanzisha Mfuko ambao utakaokuwa ni suluhisho la kimitaji na mafunzo kwa wadau wa Sekta ya Sanaa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sylvia, swali la nyongeza.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa ni jukumu la Serikali kukuza, kuibua na kuendeleza sanaa nchini, tunatambua kuna vijana wengi sana nchini wana vipaji, lakini wanashindwa kuvitumia vipaji vyao kulingana na mazingira magumu yaliyopo ya kufanya vipaji hivyo na huenda vipaji hivyo vingeweza kuwapatia ajira.

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kuibua, kuendeleza na kusimamia vipaji hivi vyta vijana walioko katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunatambua kwamba kuna taasisi na watu binafsi wanaofanya matamasha ya kuibua vipaji:-

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kuwaidia hizi taasisi au watu binafsi wanaofanya matamasha na jitihada za kusaidia kuinua vipaji Tanzania?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Sylvia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na maswali ya msingi ambayo yaliyieleka moja kwa moja kwenye swali la kwanza ambalo limeulizwa kama swali la nyongeza, Wizara yetu inajipanga vyema kutafuta vijana wenye vipaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba mimi na wasaidizi wangu tumejipanga kupita katika kila mtaa ili kuweza kutafuta vijana wenye vipaji mbalimbali. Pia, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Serikali imejipanga vizuri; na Mheshimiwa Rais tayari

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ameshaanzisha mfuko maalum ambao utawasaidia vijana wenye vipaji.

Kwa hiyo, tutapita kila mtaa, kila kijiji, kila wilaya, kila halmashauri katika kila mkoa kuhakikisha kwamba tunawasaka vijana wenye vipaji na kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili linalozungumzia matamasha yanayofanywa na baadhi ya watu na taasisi, sisi kama Wizara hatutakuwa na jambo dogo. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Wizara haitakuwa na jambo dogo, kila jambo litakuwa na uzito wake. Kwa hiyo tutashiriki katika kila kitu kinachofanyika kinachohusu utamaduni, sanaa na michezo ambacho wenzetu katika taasisi mbalimbali wamekuwa wakitusaidia Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa commitment nzuri kwa vijana wetu. Nimemwona Mheshimiwa Londo Mbunge wa Mikumi.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa sanaa imekuwa chanzo kikuu cha ajira kwa vijana wetu, je, Serikali haioni kuwa umefika wakati sasa wa kutumia vyuo vyetu vya VETA kama vituo vya kuibua na kuendeleza vipaji vya sanaa kwa vijana wetu?

Na pili...

MWENYEKITI: Swali moja Mheshimiwa.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, okay, nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa majibu ya swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi, mchapa kazi kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri mzuri aioutoa kuhusu matumizi ya vyuo vya VETA, lakini sisi kama Serikali tunakwenda mbele zaidi. Tunategemea kutumia baadhi ya shule tulizonazo kutengeneza *academy* mbalimbali. Tutatumia shule aidi ya 56 ambazo Serikali imejipanga kuzitumia kwa ajili ya kuendeleza na kukuza vipaji katika maeneo hayo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Kuhaga Joelson Mpina.

Na. 14

Ujenzi wa Bwawa la Nyerere

MHE. LUHAGA J. MPINA Aliuliza:-

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la kufua umeme wa maji la Julius Nyerere?

(b) Je, kwa nini Mkandarasi ameshindwa kujaza maji kwenye Bwawa kufikia tarehe 15 Novemba, 2021 kama illiyokuwa imekubalika?

(c) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kutohana na ucheleweshwaji huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu, nami kabla ya kujibu swali nimshukuru sana Mwenyekiti Mungu kwa afya na amani, lakini pia nimshukuru Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuhudumu katika nafasi hii ya Naibu Waziri wa Nishati. Pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wenzangu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wote kwa uchaguzi mkubwa, wa maajabu na wa furaha tuliofanya jana hapa Bungeni wa kumchagua Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisese lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa kukamilika kwa mradi kimkataba ni tarehe 14 Juni, 2022. Tarehe hiyo bado hajafikiwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili bwawa la Mwalimu Julius Nyerere lianze kujazwa maji, ni sharti liwe limejengwa kufikia kimo cha mita 95 juu ya usawa wa bahari ambapo kazi hiyo imekamillka. Aidha, illtakiwa handaki lillolengwa kuchepusha maji ya Mto Rufiji kuzibwa. Kazi ya kuziba au kufunika handaki kwa kutumia vyuma maalum vizito ilihitaji mfumo maalum ambaao ni wa kudumu wa mitambo ya kubebeta milango hiyo (*Hoist Crane system*) kuwepo katika eneo la mradi. Mfumo huo unatengenezwa mahsus kwa ajili ya kazi hii na kazi hii inapoisha *crane* hizo huondolewa na hazitumiki kwa kazi nyingine. Mitambo hiyo ilichelewa kufika kwa wakati kutohana na viwanda kufungwa na safari za meli kuathiriwa kutohana na UVIKO 19. Milango na mtambo wa kubebeta tayari imefika na kazi za kuifunga zinatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2022.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na *TANESCO* inaendelea kumsimamia mkandarasi aongeze kasi ya utekelezaji wa ujenzi ili kufidia muda uliopotea kwa kuongeza wafanyakazi na muda wa kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Luhaga Mpina, swali la nyongeza.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaauliza swali langu la nyongeza nimeshindwa kujizuia kumpongeza Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kwa kura

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

zote kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mwenyezi Mungu ambariki ili ateketeze haki za Watanzania hapa Bungeni. Baada ya hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa majibu haya yaliyotolewa, mrai wetu huu wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere hauwezi kukamilika kama mkataba ulivyosema. Tulipokuwa kwenye Kamati ya Bajeti mwezi wa 11 Waziri alikuja mbele ya Kamati akaieleza kwamba sababu za mradi huu kucheleva ni Mkandarasi kukaidi dizaini iliyowekwa na wataalam ya kujenga mahandaki matatu kwa ajili ya kuchepusha maji, lakini badala yake alijenga handaki moja, jambo ambalo lilimfanyaachelewe sana kukamilisha kazi hiyo, kwa hiyo sababu kubwa ya msingi; na sababu za UVIKO-19 zilikataliwa; na majibu haya yako kwenye *Hansard* za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tena wamekuja na majibu mengine, wanasema kwamba ni kucheleva kwa mitambo ya kubebaa ile milango ya vyuma (*hoist crane system*), ndiyo iliochelewa kufika na mradi huu kucheleva kwa sababu ya UVIKO-19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu majibu haya yanakanganya, kwenye Kamati chini ya Hansard waliyakataa majibu hayo kwamba hayana ukweli wowote na wakasema kwamba majibu sahihi ni kwamba huyo alikuwa mzembe na kwamba watam-*penalize* kwa ucheleweshaji atakaoufanya wa kuchelewesha mradi huu ambaao unacheleweshwa na Watanzania. Sasa Mheshimiwa Waziri atuambie; Kamati ni sehemu ya Bunge, na hapa wamekuja na majibu mengine, na ushahidi wa *Hansard* upo. Nini majibu ya Serikali ya kuchelewesha mradi huu, kwa sababu majibu mawili tayari yametolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kuhusu katakata ya umeme inayoendelea na mgao wa umeme unaoendelea hivi sasa. Mwanzo tulielezwa kwamba sababu ya mgao wa umeme unaoendelea sasa hivi ni kwa sababu

ya matengenezo ambayo hayakufanyika kwa miaka mitano, ndiyo maana wako kwenye *maintenance*. Baada ya muda mfupi tena tukaambiwa kwamba ni kwa sababu ya mabwawa yanayotumika kufua umeme kukauka na yamekauka kwa sababu ya mifugo pamoja na ukaidi wa binadamu. Sasa hivi tena, wakati huo huo *TANESCO* nao wanasema kwamba hakuna mgao wa umeme, baadaye *TANESCO* wanatangaza mgao wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu tuelezwe na Serikali; kwa sababu suala la katakata ya umeme na mgao wa umeme hivi sasa linaathiri sana Watanzania; viwanda vinafungwa, wananchi wako kwenye dhiki kubwa, huduma za afya zimevurugika, huduma za maji zimevurugika. Kwa ujumla Taifa liko kwenye hali ngumu ya ukosefu wa umeme...

MWENYEKITI: Umeeleweka Mheshimiwa, umeeleweka.

MHE. LUHAGA J. MPINA: ...tupate majibu sahihi ya Serikali ni nini kinachosababisha hali hii ya kukatikakatika kwa umeme kuendelea?

MWENYEKITI: Umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu hayo ili tuweke sawa masuala hayo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze na swali la kwanza, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, mradi kwa mujibu wa mkataba unatarajiwa kukamilika tarehe 14 Juni, 2022. Wazungu wanasema *do not cross the river before you reach there*. Muda utakapofika kama mradi hautakamilika hatua za kisheria za kimkataba zitachukuliwa kwa aliyesababisha ucheleweshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, lilikuwa linajitegemea, liliulizwa kwa nini maji hayakujazwa kufikia mwezi Novemba na sababu za kueleza kwamba *cranes* na milango vilichelewa kwa sababu ya UVIKO ni sababu pekee ya kuchelewesha kuziba *diversion channel* iliyokuwa inachepusha maji. Kwa hiyo maelezo hayo hayahusiani na

mradi mzima, kwamba mradi umechelewa. Kama nilivyosema, muda wa kukamilisha mradi bado haujafika na tutakapofikia mto tutaivuka kutokana na mazingira yatakayokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hakuna taarifa zinazokinzana, isipokuwa taarifa zote hizi kwa pamoja zitashughulikiwa kulingana na muda utakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, kuhusu kukatika kwa umeme; kwanza niombe kutoa maelezo ya Serikali, kwamba *TANESCO* haikatikati umeme, hakuna mtu ambaye amejiriwa kwa ajili ya kukata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo ya umeme ina-*respond*kulingana na mazingira. Kikubwa zaidi kinachotokea ni kwamba pale ambapo mitambo yetu inazidiwa na matumizi yenye *automatically* inakata umeme. Sasa tunapokwenda kuangalia tatizo ni nini, tukilibaini basi tunawasha. Mionganoni mwa tatizo ambalo limekuwa likitokea ni kwamba, mara nyingi mitambo inapokuwa imepata mzigو mkubwa ikakata umeme na wale watumiaji nao wenyewe wanazima vifaa vyao.

Kwa hiyo sisi tukirudi kwenye mtambo wetu tukawasha unakubali kuwaka kwa sababu mitambo inakuwa haipo. Sasa wale wenzetu wakiwasha tena inakata tena. Kwa hiyo pengine inaonekana kama kuna mtu anakata na kuwasha, lakini ni *system* yenye ina-*respond*. Tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvu zetu za mitambo ili kuweza ku-*capture* sasa mahitaji tulionayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala la kwamba tulisema maji, sasa tukasema gesi. Ni kwamba tulitarajia kuwa kwenye marekebisho ya mtambo yetu ya kufua gesi ambayo inazalisha sehemu kubwa sana ya umeme hapa nchini tuiongeze kwa sababu sasa tuna uwezo wa kuongeza *megawatt* takriban 290, twende tukarekebishe kwenye visima vyetu vya gesi ili sasa tuweze kupata gesi nyingi zaidi kwa sababu ya kutokuwa na hali nzuri ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme. Ule mgao au matarajio makubwa ya mgao tuliodhani tutakuwa nao hatutakuwa nao; na sababu kubwa za kutokuwa na mgao huo ni tatu. Jambo la kwanza, tumekaa pamoja na wataalam, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba mgao usiwe mkali kiasi kile, tukabaini kwamba tunaweza tukapata ile gesi iliyokuwa kwa wenzetu wa *PAETambao* ndio watakaokwenda kurekebisha mitambo yao, tukapitisha baadhi ya kiwango kidogo cha gesi kupitia mitambo yetu ya *TPDC* na hivyo kufidia upungufu wa gesi ambao tungueupata. Hiyo imekuwa ni sababu ya kwanza, kwamba lile pengo kubwa ambalo tungelipata kwa kutokuwa na gesi tutalipunguza kupitia gesi na kuichepusha kwa kupitia njia ya *TPDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tunalionia, sisi sote ni mashahidi kwa sasa, hali yetu ya mabwawa imeanza kurudi katika hali nzuri na hivyo itaweza kutusaidia kujazia sasa kwenye maeneo ambayo yanatakiwa yapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, umeme ni *supply and demand*. Tulitarajia kwamba kutakuwa kuna mahitaji makubwa sana ya umeme. Kuna kitu kinaitwa *load flow analysis*. Yulipoifanya *load flow analysis* tulibaini kwamba kile tulichokitaratja kitahitajika sicho ambacho kitahitajika. Baada ya kuwa tunahitaji takriban 280 hadi 300 tunaona zitakazohitajika ni kama *megawatt* 100, ambazo katika mfumo wa kawaida huwa hazipo hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe kauli ya Serikali, ule mgao ambao tuliutarajia utakuwepo kwa makali yale na ukubwa ule hautakuwepo na tutahakikisha kwamba watu wanaendelea kupata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niseme, katika kipindi hiki ambako kutakuwa na mgao mdogo au kutokuwepo kwa umeme katika maeneo mbalimbali tutaitumia vizuri nafasi hiyo ili kufanya mambo kadhaa yanayoboresha mfumo wetu. Mojawapo ni kuhakikisha

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tunapunguza mzigo katika njia za umeme tunazozita *feeder*, zile ambazo zimezidiwa kutoa sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kukatia miti na mapori ambayo yamekuwa yakiangukia maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuboresha vituo vyetu vya kupoza umeme. Kama jana tulifanya cha Muhimbili, leo tunafanya pale Kunduchi na kesho kutwa watafanya pale Ubungo ili kuhakikisha kwamba tutakaporudi katika hali ya kawaida baada ya wiki moja ama mbili, tunarudi katika hali nzuri ambayo itakuwa bora kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, na nafikiri Waheshimiwa Wabunge tutakubaliana kwamba maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mpina yamewagusa Wabunge wengi katika maeneo yao. Kwa hiyo naomba tuendelee kuiamini Serikali na kauli pamoja na *commitment* ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya mwisho ambayo ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Khadija, Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum aulize swalı lake.

Na. 15

**Mgawanyo wa Vitabu vya Nukta Nundu Chini ya
Fedha za Mapambano Dhidi ya UVIKO-19**

MHE. KHADIJA S. TAYA aliuliza:-

Je, ni upi mgawanyo wa vitabu 812 vya nukta nundu vilivyotolewa katika Mpango wa Fedha za Mapambano dhidi ya UVIKO 19?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nichukue fursa hii adhimu na adimu kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu alitupa kibali cha kukutana katika eneo hili kwa siku ya leo. Shukrani ya pili nimpelekee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu, Mama Samia Suluhu Hasan kwa kuendelea kuniamini na kutuamini sisi, mimi na Profesa Mkenda kuweza kumsaidia katika eneo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayasi na Teknolojia, kujibu swalii la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa vitabu vya Nukta Nundu kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi wasioona kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wasioona wapatao 514 wanaosoma katika shule za sekondari nchini, Serikali kuitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 ilitenga shilingi milioni 704 kwa ajili ya kuchapajumla ya nakala 18,200 za vitabu kwa ajili ya wanafunzi wasioona vya masomo yote ya sekondari, ambapo nakala 9,100 ni vitabu vya nukta nundu na nakala 9,100 ni vitabu vya michoro.

Mheshimiwa Spika, uchapaji wa vitabu hivyo upo katika hatua za mwisho na utakapokamiliika vitasambazwa katika mikoa yote kulingana na mahitaji. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika mikoa yote wakiwemo wanafunzi wasioona. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khadija Taya.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba niipongeze Serikali kwa majibu mazuri na wameonesha kabisa kwamba mmeongeza vitabu. Pamoja na hayo yote naomba niongeze swali la kuhusu watu wenye uoni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye uoni hafifu shulenii wanapata taabu sana, kwa sababu Walimu wengi hawafahamu namna ya kuwafundisha hawa watu ili waweze kuelewa. Wanapata tabu ubaoni na kwenye karatasi kwa sababu maandishi yanakuwa ni madogo. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka mwongozo kwenye shule zote na Walimu wote wafahamu namna gani ya kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum, hasa hao wenye uoni hafifu ambao wengi ni wenye ulemavu wa ngozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunafahamu kabisa, katika suala la afya na maradhi watu wenye ulemavu wanapata shida sana na wanapata maradhi kutokana na hali ya usafi na mazingira pale shulenii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu, kuongeza vyoo vya watu wenye ulemavu shulenii ili hawa watu waweze kusoma vizuri? Kwa sababu tunaamini kabisa kwamba elimu ndio ufunguo wa maisha na elimu ndiyo mkombozi wa watu wote wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khadija taya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayoyazungumza Mheshimiwa, kwamba wenzetu wenye uoni hafifu, hasa wenzetu wenye ulemavu wa ngozi wanapata changamoto shulenii. Naomba nimhakikishie Mheshimwia Mbunge pamoja

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali yetu hii ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan tumejipanga vyema katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kuishughulikia changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Wizara iko mbioni kutekeleza au kukamilisha mwongozo ambao utakwenda kushughulikia eneo hili la wanafunzi wetu wenye changamoto ya uoni hafifu, tukishirikiana na wenzetu wa Shirika Binafsi la *Under the Same Sun*. Kwa hiyo nimwondoe kabisa wasiwasi, kwamba mwongozo huo uko mbioni kuja na mara utakapokamilika na kusainiwa tutausambaza kwenye maeneo hayo ili kuhakikisha kwamba tunaitatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie vile vile Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yetu tayari imeweza kusambaza vitabu vyenye maandishi makubwa kwa ajili ya wenzetu hawa ambao wana uoni hafifu. Kwa hiyo kule kwenye shule zetu zote za msingi pamoja na sekondari mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anazungumzia suala la miundombinu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mgawanyo wa fedha za UVIKO-19, zile ambazo tulizipata kupitia Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI zaidi ya Shilingi bilioni 2.4 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo zaidi ya 2200 kwa ajili ya wanafunzi wetu wenye mahitaji maalum kupitia hizi za UVIKO-19 na zile za *GPE lenses* na mchakato huu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kupitia mradi wetu wa *EP4R* umeweza kujenga jumla ya matundu 4,549 kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule zetu za msingi na sekondari. Tunaendelea kuboresha miundombinu hii kwa kuhakikisha na wao tunawatengenezea mazingira wezeshi ili isiwe changamoto kwao katika kupata elimu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na hilo ndilo swalii letu la mwisho kwa siku ya leo na muda wetu umemalizika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wetu umekwisha na kazi yetu ya leo imekwisha, basi nawashukuru na kuwapongeza kwa kuwajibika ipasavyo. Niendelee kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kujitahidi kuuliza maswali mafupi ya Kibunge na Mawaziri kujibu majibu mafupi ya Kibunge ili Wabunge wengi tuweze kupata fursa ya kuuliza kwa ajili ya majimbo yetu.

Baada ya kusema hayo, basi naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.10 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 3 Februari, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*